# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## MAFUNZO YA UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI MSIMU 2023/2024 KWA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI.

**Bodi ya Korosho Tanzania (CBT)** inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba itaendesha mafunzo ya Uhakiki Ubora kuanzia tarehe **11/09/2023 hadi 15/09/2023** katika ukumbi wa Mikutano wa Chuo cha Kilimo Mtwara (MATI). Mafunzo haya yanatolewa kwa mujibu wa kifungu namba 20(1) cha sheria namba 18 ya mwaka 2009 ya korosho na kanuni za mwaka 2010.

Mafunzo ya udhibiti ubora yatatolewa kwa watu wote wanaofanya kazi ama wenye nia ya kufanya kazi za uhakiki ubora katika msimu wa mauzo ya Korosho kwa mwaka 2023/2024. Mafunzo hayo yanalenga Wataalam wapya katika Tasnia ya korosho na wale wadau wote wa korosho ambao wanataka kujifunza kuhusu ubora wa korosho, wakiwemo wataalam wa Waendesha Ghala, Wanunuzi, Vyama Vikuu vya Ushirika, Wamiliki wa Viwanda vya kubangua Korosho,Wataalam wa Ugani na Kilimo, Vyama vya msingi n,k.

**Sifa za Mshiriki**:

- Mdau katika Tasnia ya Korosho mwenye nia ya kupata elimu ya udhibiti ubora wa korosho ghafi.
- Mtu mwenye elimu ya kilimo au taaluma zinazo shabihiana na kilimo atakuwa na sifa kufanya kazi kwenye ghala za korosho nchini.

Gharama ya ushiriki wa mafunzo na kupatiwa cheti ni **Sh. 300,000.** Aidha, Wataalam kwenye ghala wenye vyeti vya miaka ya nyuma pamoja na Mameneja wa ghala zote nchini wanawajibika kuhudhuria bila kukosa siku ya tarehe 15/09/2023 kwa ajili ya kupata taratibu (*update)* za msimu2023/2024 na mafunzo ya mfumo wa utoaji vibali vya kusafirishia korosho ghafi kwa gharama ya **Sh. 50,000/=** kwa kila mmoja katika akaunti tajwa hapo chini.

***Benki: CRDB,*** *Jina la Akaunti****: CBT cashewnut a/c 1992/93****, Akaunti namba* ***01J1015826005.***

Kwa maelezo zaidi fika katika ofisi za Bodi ya Korosho Tanzania Makao Makuu –Mtwara (au wasiliana kwa kutumia simu namba (**0800 112159**), au katika matawi yaliyopo Tunduru, Dar es salaam, Tanga na Manyoni. Malipo yote yafanyike kupitia benki. Mwisho wa kupokea malipo ni tarehe **08/09/2023 saa 10:30 jioni**, baada ya kulipia hakikisha unatunza nakala yako ya malipo na kuja nayo siku ya mafunzo.

**Angalizo:**
Katika msimu wa mavuno 2023/2024, hakuna Mtaalam yoyote wa ubora atakayeruhusiwa kufanya kazi za uhakiki ubora wa korosho ghafi kwenye ghala za Minada, ghala za Wanunuzi na Viwanda vya kubangua korosho ghafi kama hajapatiwa mafunzo na cheti kutoka Bodi ya korosho.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
**S.L.P 533, MTWARA info@cashew.go.tz**
**AGOSTI, 2023.**